**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR, NAM. 3 YA 2011 NA KUTUNGA SHERIA YA BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU ZANZIBAR KWA AJILI YA KUTOA MSAADA WA KIFEDHA KWA WANAFUNZI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA KWA BODI


3. Kuanzishwa kwa Bodi.

4. Muhuri na Nembo ya Bodi.

5. Kazi za Bodi.

6. Uwezo wa Bodi.


### SEHEMU YA TATU
### USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA BODI


7. Uanzishwaji na muundo wa Bodi ya Usimamizi.

8. Kazi za Bodi ya Usimamizi.

9. Sifa za Mwenyekiti.

10. Katibu wa Bodi ya Usimamizi.

11. Mwenendo wa Bodi ya Usimamizi.

12. Mkurugenzi Mtendaji.

13. Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji.

14. Idara, vitengo na divisheni.

15. Wafanyakazi wa Bodi

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA KUTOA MKOPO

16. Kustahiki mkopo.

17. Mahitaji yanayotolewa mkopo.

18. Uhakiki na kutoa taarifa za mkopo.

19. Makubaliano ya Mkopo.

20. Wajibu wa mnufaika.

21. Wajibu wa mdhamini.

22. Maombi ya mkopo kwa mwanafunzi anayeendelea.

## SEHEMU YA TANO
## MAREJESHO YA MKOPO

23. Marejesho ya mkopo.

24. Kurejesha mkopo mapema.

25. Kulipa kwa mkupuo au kuongeza kasi ya kurejesha mkopo.

26. Wajibu wa Mwajiri.

27. Makato kutoka kwa mwajiri

28. Makato ya mkopo kuwa ya kisheria.

29. Marejesho ya mkopo kwa mnufaika asiyeendelea.

30. Kufuta, kuakhirisha au kusamehe marejesho ya mkopo.

31. Utoaji wa Cheti cha Kumaliza Mkopo.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA FEDHA


32. Fedha na rasilimali za Bodi.

33. Bajeti ya mwaka ya Bodi.

34. Hesabu na ukaguzi.

35. Ripoti ya Utekelezaji ya Mwaka.

36. Ufunguaji wa Hesabu ya Benki


## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI MENGINEYO


37. Mkopo kwa ngazi nyengine ya elimu.

38. Uwezo wa kuwekeza fedha za ziada.

39. Mnufaika kuwajibika kwa taratibu za madai.

40. Makosa na adhabu.

41. Adhabu ya jumla.

42. Mapitio na rufaa

43. Kanuni.

44. Kufuta na kubakiza.


## JADWELI

**SHERIA NAM. 2 YA 2024**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

15 Machi, 2024

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR, NAM. 3 YA 2011 NA KUTUNGA SHERIA YA BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU ZANZIBAR KWA AJILI YA KUTOA MSAADA WA KIFEDHA KWA WANAFUNZI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na Kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar, 2024 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"ajira" maana yake ni mkataba wa kutoa huduma baina ya muajiri na muajiriwa na unajumuisha mtu aliyejiajiri mwenywe;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria hii;

"Bodi ya Usimamizi" maana yake ni Bodi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7(1) cha Sheria hii;

“elimu ya juu” maana yake ni elimu inayotolewa na kupelekea kutunukiwa shahada au ngazi nyengine ya elimu kama ilivyoamuliwa na Serikali;

“kipindi cha ahueni” maana yake ni muda maalumu kwa mnufaika kuanza kulipa mkopo, kama utakavyoainishwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii;

“mdhamini” maana yake ni mtu anayemchukulia dhamana mwanafunzi kwa madhumuni ya kupatiwa mkopo chini ya masharti ya Sheria hii;

“mkopo” maana yake ni kiwango cha fedha kinachotolewa na Bodi kwa mwanafunzi kumuwezesha kulipia gharama zinazoambatana na masomo chini ya Sheria hii;

“Mkurugenzi Mtendaji” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 12(1) cha Sheria hii;

“mnufaika” maana yake ni mtu aliyepokea mkopo chini ya masharti ya Sheria hii;

“muombaji” maana yake ni mtu anayeomba mkopo katika Bodi;

“muajiri” maana yake ni mtu yeyote wa ndani au nje ya nchi ambaye amemuajiri mnufaika kwa malipo ya mshahara;

“mwanafunzi” maana yake ni mtu aliyedahiliwa katika taasisi inayotambulika kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu na anapokea mkopo kutoka kwa Bodi;

“taasisi inayotambulika” ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346 ya 2005 ya Sheria za Tanzania;

“Waziri” maana yake ni Waziri anayehusika na elimu.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA BODI

Kuanzishwa kwa Bodi.

3.-(1) Kunaanzishwa Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar.

(2) Bodi itakuwa ni chombo kinachojitegemea na chenye kurithiwa na kuwa na muhuri wake na kwa jina lake, itakuwa na uwezo, kwa mujibu wa sheria, wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kununua au kupata kwa njia nyengine, kumiliki au kuondoa mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika;

(c) kuingia kwenye mkataba au makubaliano; na

(d) kufanya au kutekeleza jambo lolote kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake chini ya masharti ya Sheria hii ambalo Bodi inaweza kufanya au kutekeleza kisheria.

Muhuri na Nembo ya Bodi.

**4.**-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Bodi katika umbile na ukubwa kama itakavyoamuliwa na Bodi ya Usimamizi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Bodi katika waraka wowote yatathibitishwa kwa saini ya Mkurugenzi Mtendaji au afisa wa Bodi aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa hati iliyotolewa na Bodi utawekwa muhuri wa Bodi na kuthibitishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Bodi.

**5.** Kazi za Bodi zitakuwa ni:

(a) kupokea na kuzingatia maombi ya mkopo kutoka kwa waombaji;

(b) kuweka vigezo, masharti na kutoa miongozo ili kuhakikisha usawa katika kutoa, kurejesha na kugomboa mkopo;

(c) kutoa mikopo kwa wanafunzi ili kuwawezesha kumudu gharama za elimu ya juu;

(d) kutafuta na kusimamia ufadhili na udhamini wa masomo ya elimu ya juu;

(e) kuweka mikakati ya kuhakikisha uthabiti, uwazi, ubora na ufanisi wa utoaji mikopo, ufadhili na udhamini wa masomo na kuweka mikakati ya kurejesha na kugomboa mkopo;

(f) kutunza daftari la kumbukumbu na taarifa nyengine za waombaji, wanafunzi, wanufaika na ufadhili wa masomo;

(g) kutafuta fedha na misaada mingine kwa ajili ya kutekeleza kazi za Bodi; na

(h) kutekeleza kazi nyengine yoyote muhimu au inayohusiana na malengo ya Bodi kama itakavyoidhinishwa na Bodi ya Usimamizi.

Uwezo wa Bodi.

**6.** Bodi itakuwa na uwezo wa:

(a) kupendekeza kiwango cha idadi ya wanafunzi watakaopatiwa mkopo, ufadhili na udhamini katika mwaka husika wa masomo;

(b) kupendekeza viwango vya mkopo vitakavyotolewa kwa wanafunzi;

(c) kutaka taarifa yoyote kutoka kwa mtu, taasisi ya serikali au binafsi kuhusiana na kazi za Bodi;

(d) kusitisha utoaji wa mkopo kwa mwanafunzi;

(e) kupendekeza ada kwa huduma zinazotolewa na Bodi; na

(f) kuanzisha ushirikiano wa kikazi na taasisi za elimu ya juu, waajiri, wadhamini na watu au vyombo vyengine vya ndani au nje ya Zanzibar kwa namna ambayo Bodi itaona ni sahihi katika kutekeleza kazi zake.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA BODI

Uanzishwaji na muundo wa Bodi ya Usimamizi.

**7.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Usimamizi ya Bodi ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mtendaji;

(c) Mjumbe kutoka:

(i) Wizara inayohusika na fedha;

(ii) Tume ya Mipango Zanzibar;

(iii) Jumuiya ya Waajiri kutoka sekta binafsi;

(iv) Shirikisho linalohusu wanafunzi wa elimu ya juu Zanzibar; na

(v) taasisi za elimu ya juu.

(2) Wajumbe wa Bodi ya Usimamizi waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) (c) cha kifungu hiki, watateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na wakuu wa taasisi husika kwa kuzingatia uzoefu, utaalamu na jinsia.

Kazi za Bodi ya Usimamizi.

**8.** Kazi za Bodi ya Usimamizi zitakuwa ni:

(a) kusimamia utawala, utekelezaji na uendeshaji wa Bodi,

(b) kupendekeza muundo wa utumishi wa Bodi;

(c) kuidhinisha mipango ya maendeleo ya Bodi;

(d) kuzingatia na kuidhinisha bajeti ya Bodi iliyowasilishwa na Mkurugenzi Mtendaji;

(e) kuajiri watumishi wa Bodi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011;

(f) kumshauri Waziri juu ya sera zinazohusiana na kazi za Bodi;

(g) kuamua kiwango cha idadi ya wanafunzi watakaopatiwa mkopo, ufadhili na udhamini katika mwaka husika wa masomo;

(h) kuamua viwango vya mkopo vitakavyotolewa kwa wanafunzi;

(i) kuamua ada kwa huduma zinazotolewa na Bodi; na

(j) kufanya kazi nyengine yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

Sifa za Mwenyekiti.

**9.** Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi, ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya elimu, uchumi, biashara, uhasibu au fani nyengine inayolingana na hizo kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba katika masuala ya uongozi; na

(c) ni muadilifu wa hali ya juu.

Katibu wa Bodi ya Usimamizi.

**10.**-(1) Bodi ya Usimamizi itamteua afisa wa Bodi kuwa Katibu wa Bodi ya Usimamizi.

(2) Afisa wa Bodi atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi ya Usimamizi, ikiwa afisa huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria au ana sifa za kuwa katibu wa shirika kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali; na

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika utumishi wa umma.

(3) Katibu atawajibika kwa Bodi ya Usimamizi na atakuwa na kazi ya:

(a) kuandaa ajenda za vikao vya Bodi ya Usimamizi baada ya kushauriana na Mwenyekiti;

(b) kuchukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi ya Usimamizi;

(c) kutunza kumbukumbu kamili na sahihi za vikao vya Bodi ya Usimamizi;

(d) kutoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi ya Usimamizi kwa wajumbe;

(e) kutoa ushauri kwa Bodi ya Usimamizi pale itakapohitajika; na

(f) kutekeleza kazi nyengine kama atakavyoelekezwa na Bodi ya Usimamizi.

Mwenendo wa Bodi ya Usimamizi.

**11.** Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi ya Usimamizi yatakuwa kama yalivyoelezwa katika Jadweli la Sheria hii.

Mkurugenzi Mtendaji.

**12.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya elimu, uchumi, biashara, uhasibu au fani nyengine inayolingana na hizo;

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba katika utumishi wa umma; na

(c) uadilifu wa hali ya juu

Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji.

**13.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Bodi na atawajibika na uendeshaji na usimamizi wa kila siku wa watumishi wa Bodi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mtendaji:

(a) atasimamia mapato, matumizi na mali zote za Bodi;

(b) atahakikisha watumishi wa Bodi wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili na uwajibikaji;

(c) atasimamia masuala ya nidhamu kwa watumishi wa Bodi; na

(d) atatekeleza jukumu jengine atakaloelekezwa na Bodi ya Usimamizi kwa mujibu wa sheria.

Idara, vitengo na divisheni.

**14.**-(1) Bodi inaweza, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, kuanzisha idara, vitengo na divisheni kama itakavyoona inafaa.

(2) Wakuu wa idara na vitengo watateuliwa na Bodi ya Usimamizi kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(3) Wakuu wa divisheni watateuliwa na Mkurugenzi Mtendaji kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(4) Wakuu wa idara, vitengo na divisheni katika kutekeleza kazi zao watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji.

Wafanyakazi wa Bodi

**15.** Bodi ya Usimamizi, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, itaajiri wafanyakazi wa Bodi kama itakavyokuwa ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Bodi.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA KUTOA MKOPO

Kustahiki mkopo.

**16.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, muombaji atastahiki kupata mkopo ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) amedahiliwa katika taasisi inayotambulika na kuchagua programu ya mafunzo inayoendana na Mpango wa Vipaumbele wa Taifa; na

(c) amethibitika kutokuwa na msaada wa kifedha kutoka vyanzo vyengine kugharamia mahitaji yote au sehemu ya mahitaji kwa kitu ambacho maombi yamefanywa.

(2) Mnufaika anayeomba mkopo kwa ngazi ya masomo ya juu zaidi ya ngazi aliyopewa mkopo anastahiki kupata mkopo huo ikiwa amerejesha mkopo wake kwa asilimia iliyoainishwa katika kanuni.

(3) Bodi inaweza, kwa tangazo litakalochapishwa au kutangazwa katika chombo cha habari chochote kilichosambaa sehemu kubwa ya nchi, kutangaza programu za masomo zitakazotolewa mkopo kwa mwaka wa masomo husika.

(4) Taratibu za kuomba mkopo zitaelezwa katika muongozo utakaotolewa na Bodi.

Mahitaji yanayotolewa mkopo.

**17.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itatoa, kwa njia ya mkopo, fedha kwa ajili ya:

(a) ada za masomo;

(b) ada za mtihani;

(c) vyakula na malazi;

(d) vitabu na vifaa vya kuandikia;

(e) posho ya usafiri;

(f) gharama za utafiti;

(g) gharama za mafunzo ya vitendo;

(h) mahitaji maalumu ya kitivo;

(i) gharama za matibabu;

(j) mahitaji na visaidizi kwa watu wenye ulemavu; na

(k) mahitaji mengine kama itakavyoamuliwa na Bodi ya Usimimizi.

(2) Bodi itatoa mkopo kwa kuzingatia mahitaji yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kwa kiasi itakachoamua.

(3) Endapo Bodi itatoa mkopo kwa mahitaji au kiwango pungufu ya vitu vilivyoainishwa au kuombwa, sehemu ya mahitaji au kiasi kilichobaki kitabebwa na mwanafunzi.

Uhakiki na kutoa taarifa za mkopo.

**18.**-(1) Bodi, baada ya kupokea ombi, itahakiki taarifa zilizomo kwenye ombi lililowasilishwa.

(2) Bodi itamuarifu muombaji kuhusiana na ombi lake kabla ya kuanza kwa mwaka wa masomo ulioombewa mkopo.

(3) Taarifa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, itakuwa kama itakavyoelezwa katika muongozo utakaotolewa na Bodi.

Makubaliano ya Mkopo.

**19.**-(1) Bodi itaingia Makubaliano ya Mkopo na mwanafunzi kwa kuzingatia mahitaji yanayotolewa mkopo.

(2) Vigezo na masharti ya Makubaliano ya Mkopo yataelezwa katika kanuni.

Wajibu wa mnufaika.

**20.** Mnufaika atapaswa, baada ya kipindi cha ahueni au ndani ya kipindi kitakachoamuliwa na Bodi ya Usimamizi:

(a) kuijuilisha Bodi anuani yake ya mawasiliano;

(b) kuanza kurejesha mkopo; na

(c) ikiwa ameajiriwa, kumpa taarifa mwajiri wake kukata kiwango cha fedha kutoka katika mshahara wake na kukiwasilisha kwa Bodi kwa namna ambayo Bodi ya Usimamizi itaelekeza.

Wajibu wa mdhamini.

**21.**-(1) Mwanafunzi atakuwa na wadhamini wawili kabla ya kupatiwa mkopo.

(2) Mdhamini atalazimika, yeye mwenyewe au baada ya kutakiwa na Bodi:

(a) kuijulisha Bodi anuani ya makaazi na kazi ya mnufaika;

(b) kuhakikisha kwamba mnufaika anarejesha mkopo ambao anawajibika kuulipa; na

(c) kutoa taarifa yoyote muhimu kuhusu mnufaika.

(3) Vigezo vya mdhamini vitaelezwa katika kanuni.

Maombi ya mkopo kwa mwanafunzi anayeendelea.

**22.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi, kupitia muongozo, itaainisha masharti ya ziada kwa ombi la mkopo kwa mwanafunzi anayeendelea.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "mwanafunzi anayeendelea" inajumuisha mwanafunzi ambaye:

(a) anaendelea na programu ya masomo kwa mwaka wa masomo unaofuata;

(b) anarudia mwaka wa masomo kwa sababu yoyote;

(c) amesitishwa kuendelea na masomo na anatarajia kuomba masomo katika taasisi nyengine inayotambulika; au

(d) amebadili taasisi inayotambulika au programu ya masomo ambayo mkopo umetolewa.

## SEHEMU YA TANO
## MAREJESHO YA MKOPO

Marejesho ya mkopo.

**23.**-(1) Mnufaika ataanza kurejesha mkopo baada ya kumalizika kipindi cha ahueni ambacho mkopo ulitolewa kwa mujibu wa Mkataba wa Mkopo.

(2) Kwa ajili ya kuondoa shaka, masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hayatatumika kwa mnufaika mwenye ajira.

(3) Mnufaika chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki atapaswa kurejesha mkopo katika kipindi kitakachoamuliwa na Bodi.

(4) Bodi, ndani ya siku thelathini baada ya muda ulioainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kumalizika, itamuarifu mnufaika kuanza kurejesha mkopo.

(5) Endapo mnufaika hatokuwa na kipato cha kurejesha mkopo, atalazimika ndani ya siku thelathini baada ya kupokea taarifa ya kuanza kurejesha mkopo kuijulisha Bodi kwa maandishi juu ya sababu ya kushindwa kurejeshwa mkopo huo.

(6) Bodi inaweza, baada ya kuhakiki taarifa chini ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, kuongeza muda wa kurejesha mkopo kwa mnufaika huyo.

(7) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mnufaika anaweza kulipa mkopo kwa mkupuo au kwa namna atakavyoamua.

(8) Mnufaika anayekwenda kinyume na kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

**Kurejesha mkopo mapema.**

**24.**-(1) Mwanafunzi au mnufaika anaweza kurejesha mkopo mapema kwa utaratibu utakaoamuliwa na Bodi.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "kurejesha mkopo mapema" inatumika kwa:

(a) malipo ya mkopo kabla ya kumalizika programu ya masomo ambayo mkopo unatolewa; au

(b) malipo ya mkopo kabla ya kumalizika kipindi cha ahueni.

**Kulipa kwa mkupuo au kuongeza kasi ya kurejesha mkopo.**

**25.**-(1) Bila ya kujali masharti ya Sheria hii, mnufaika anaweza kulipa kwa mkupuo au kuongeza kasi ya kurejesha mkopo kwa namna atakavyoamua na kuitaarifu Bodi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi inaweza, kwa namna kama itakavyoelezwa katika kanuni, kutoa punguzo kwa mnufaika aliyerejesha mkopo kwa mkupuo au aliyeongeza kasi ya kurejesha mkopo.

**Wajibu wa Mwajiri**

**26.**-(1) Kila mwajiri, ndani ya siku tisini kutoka tarehe ya ajira, kuwasilisha kwa Bodi taarifa za waajiriwa wapya kwa ajili ya kuwatambua wanufaika chini ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, wajibu wa kuwasilisha taarifa kwa Bodi utatumika pia kwa mwajiri katika sekta binafsi ndani na nje ya Zanzibar.

**Makato kutoka kwa mwajiri.**

**27.**-(1) Mwajiri, ndani ya kila mwezi, atakata na atawasilisha kwa Bodi kiwango cha fedha kilichoainishwa na Bodi kutoka katika mshahara wa mnufaika.

(2) Bodi inaweza kumuelekeza mwajiri kukata kiwango cha fedha kutoka katika mshahara wa mnufaika endapo mwajiri au mnufaika hatoijulisha Bodi kuhusu ajira ya mnufaika.

Makato ya mkopo kuwa ya kisheria.

**28.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, makato ya mkopo yatakuwa ni ya kisheria.

(2) Bodi itaamua kiwango au asilimia ya makato ya mkopo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Marejesho ya mkopo kwa mnufaika asiyeendelea.

**29.**-(1) Bila ya kujali masharti ya Sheria hii, mnufaika asiyeendelea atawajibika kurejesha mkopo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, maneno "mnufaika asiyeendelea" maana yake ni mnufaika:

(a) aliyesitisha masomo kwa sababu yoyote kabla ya kukamilika kipindi ambacho mkopo umetolewa; au

(b) anayeendelea na masomo lakini hakusudii kuendelea kupokea mkopo zaidi kutoka Bodi.

Kufuta, kuakhirisha au kusamehe marejesho ya mkopo.

**30.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016, Bodi inaweza kusamehe deni la mnufaika ikiwa mnufaika:

(a) amefariki; au

(b) amepoteza uwezo wa kufanya kazi kimwili au kiakili kwa mujibu wa sheria yoyote inayohusika.

(2) Waziri kupitia kanuni ataeleza mazingira ya kuakhirisha kurejesha mkopo.

(3) Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya fedha na kwa tangazo litakalochapishwa katika Gazeti, kusamehe kundi lolote la wanufaika, sehemu au mkopo wote chini ya Sheria hii ambapo kwa maoni yake, kufanya hivyo ni kwa ajili ya maslahi ya umma.

Utoaji wa Cheti cha Kumaliza Mkopo.

**31.**-(1) Bodi, baada ya mnufaika kumaliza marejesho ya mkopo, itatoa Cheti cha Kumaliza Mkopo ambacho kitakuwa ni uthibitisho unaojitosheleza wa kumaliza marejesho ya mkopo wote.

(2) Taarifa kuhusu cheti kilichotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatolewa kwa muajiri au mdhamini kadri itakavyokuwa.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na rasilimali za Bodi.

**32.** Fedha na rasilimali za Bodi zitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha kwa ajili ya kutoa mkopo;

(c) fedha au rasilimali zilizopokelewa na Bodi kutokana na ada, msaada, zawadi au mfumo mwengine wowote;

(d) fedha zilizopokelewa na Bodi kutokana na marejesho ya mkopo au huduma nyengine zinazotolewa na Bodi;

(e) fedha zitakazopokelewa kutokana na uwekezaji uliofanywa na Bodi; na

(f) fedha nyengine zozote zitakazopatikana kihalali.

Bajeti ya mwaka ya Bodi.

**33.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji, si chini ya miezi mitatu kabla ya kumalizika kila mwaka wa fedha, ataandaa bajeti ya mwaka inayoonesha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata na kuiwasilisha kwa Bodi ya Usimamizi kwa kupata ridhaa na kuiwasilisha kwa Waziri.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, Bodi inaweza, wakati wowote kuandaa bajeti ya ziada kwa mwaka wa fedha unaoendelea na kuiwasilisha kwa Bodi ya Usimamizi kwa kupata ridhaa na kuiwasilisha kwa Waziri.

Hesabu na ukaguzi.

**34.**-(1) Bodi itatunza vitabu na kumbukumbu kamili za miamala yote kwa lengo la kuhakikisha kuwa fedha zote zilizopokelewa au kulipwa na Bodi zinahesabiwa kwa usahihi.

(2) Taarifa za mwaka za fedha za Bodi zitakaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016 na sheria nyengine zozote za fedha.

Ripoti ya Utekelezaji ya Mwaka.

**35.**-(1) Bodi, ndani ya miezi mitatu baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha, itaandaa na kuwasilisha kwa Bodi ya Usimamizi kwa kupata ridhaa na kuiwasilisha kwa Waziri Ripoti ya Utekelezaji ya Mwaka.

(2) Ripoti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki itatoa taarifa kamili kuhusiana na shughuli za Bodi katika mwaka wa fedha unaohusiana nayo, na itajumuisha:

(a) nakala ya taarifa ya hesabu za Bodi zilizokaguliwa pamoja na ripoti ya mkaguzi;

(b) ripoti ya utekelezaji ya Bodi ya mwaka wa fedha huo; na

(c) taarifa nyengine muhimu ya Bodi kama Waziri atakavyohitaji.

(3) Kwa ajili ya umma kupata taarifa na baada ya kupata ridhaa ya Waziri, Bodi inaweza kuchapisha na kusambaza Ripoti ya Utekelezaji ya Mwaka kwa utaratibu utakaoamua.

Ufunguaji wa Hesabu ya Benki.

**36.** Bodi, kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, itafungua Hesabu ya Benki na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake kwa mujibu wa Sheria hii.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI MENGINEYO

Mkopo kwa ngazi nyengine ya elimu.

**37.**-(1) Bila ya kujali masharti ya Sheria hii, Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Bodi ya Usimamizi na kwa tangazo lililochapishwa katika Gazeti, kutoa mkopo kwa ngazi nyengine ya elimu ambapo kwa maoni yake ni kwa maslahi ya umma.

(2) Utaratibu wa utoaji, urejeshaji na ugomboaji wa mkopo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki utaainishwa katika kanuni.

Uwezo wa kuwekeza fedha za ziada.

**38.** Kwa kuzingatia sheria yoyote inayohusika, Bodi inaweza kuwekeza fedha za ziada.

Mnufaika kuwajibika kwa taratibu za madai.

**39.** Endapo mnufaika ana uwezo wa kurejesha mkopo na bila ya sababu za msingi anashindwa kurejesha mkopo atachukuliwa kuwa ameshindwa kurejesha mkopo wake na atawajibika kwa taratibu za madai.

Makosa na adhabu.

**40.**-(1) Mtu ambaye:

(a) ametoa taarifa za uongo kwa Bodi;

(b) ameshindwa kukata na kuwasilisha kwa Bodi kiwango cha fedha kutoka katika mshahara wa muajiriwa ambaye ni mnufaika baada ya kupewa taarifa na Bodi;

(c) ameshindwa kutoa taarifa zilizotakiwa na Bodi,

ametenda kosa na akitiwa hatiani:

(i) ikiwa ni mtu binafsi, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Tanzania Milioni Moja na isiyozidi Shilingi za Tanzania Milioni Tatu; na

(ii) ikiwa mtu huyo ni chombo kinachojitegemea, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Tanzania Milioni Tatu na isiyozidi Shilingi za Tanzania Milioni Tano.

(2) Bila ya kujali sheria nyengine yoyote, endapo mwajiri ni chombo kinachojitegemea, afisa mtendaji mkuu wa chombo hicho anaweza kuwajibika binafsi.

Adhabu ya jumla.

**41.** Mtu ambaye amekwenda kinyume na masharti yoyote ya Sheria hii ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyotolewa kwa kosa hilo, ametenda kosa, na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi za Tanzania Laki Moja lakini isiyozidi Shilingi za Tanzania Milioni Moja.

Mapitio na rufaa.

**42.**-(1) Mtu yeyote asiyeridhika na uamuzi wa Bodi anaweza, ndani ya siku kumi na nne, kuwasilisha malalamiko kwa Bodi ya Usimamizi kwa mapitio.

(2) Mtu asiyeridhika na mapitio chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, anaweza ndani ya siku kumi na nne kukata rufaa kwa Waziri ambaye uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

(3) Utaratibu wa mapitio na rufaa utaelezewa katika kanuni.

Kanuni.

**43.**-(1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga kanuni kueleza:

(a) taratibu za kuomba na kutoa mkopo;

(b) taratibu za kurejesha, kugomboa na kurejesha mkopo mapema;

(c) mazingira ya kuakhirisha kurejesha mkopo;

(d) taratibu za kurejesha mkopo kwa mwanafunzi anaeyendelea;

(e) vigezo vya mdhamini;

(f) vigezo na masharti ya makubaliano ya mkopo;

(g) utaratibu wa kushughulikia mapitio na rufaa;

(h) utaratibu wa utoaji, urejeshaji na ugomboaji mkopo kwa ngazi ya stashahada; na

(i) ada zinazolipwa kwa huduma zinazotolewa na Bodi chini ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza..

**44.**-(1) Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, Nam. 3 ya 2011 inafutwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa au kukusudiwa kufanywa chini ya Sheria iliyofutwa, litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI

---

## MWENENDO WA BODI YA USIMAMIZI
**[Chini ya kifungu cha 11]**

---

*Makamu Mwenyekiti.*

**1.** Wajumbe wa Bodi ya Usimamizi, katika kikao cha kwanza, watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti.

*Muda wa Bodi ya Usimamizi.*

**2.** Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi ya Usimamizi, watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

*Vikao vya Bodi ya Usimamizi.*

**3.**-(1) Bodi ya Usimamizi itakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu kwa mkutano wa kawaida na inaweza kukutana katika vikao vya dharura wakati wowote itakapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi ya Usimamizi vitaongozwa na Mwenyekiti, na ikiwa hayupo vitaongozwa na Makamu Mwenyekiti na ikiwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wote hawapo, wajumbe waliopo watamchagua mmoja miongoni mwao kuongoza kikao.

*Akidi.*

**4.** Akidi ya kikao cha Bodi ya Usimamizi itakuwa zaidi ya nusu ya idadi yote ya wajumbe wake.

*Uamuzi wa Bodi ya Usimamizi*

**5.** Bodi ya Usimamizi itafanya uamuzi wake kwa makubaliano ya wajumbe, na ikitokea kutokukubaliana, uamuzi utafikiwa kwa kura na iwapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

*Taratibu za vikao.*

**6.** Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, Bodi ya Usimamizi itakuwa na uwezo wa kuandaa taratibu zake zenyewe kuhusiana na vikao na utaratibu wa kutekeleza shughuli zake ikijumuisha Kamati za Bodi ya Usimamizi.

*Mjumbe mualikwa.*

**7.** Bodi ya Usimamizi inaweza kumualika mtu yoyote kushiriki majadiliano ya kikao cha Bodi ya Usimamizi kama mtaalamu lakini mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

*Kumbukumbu za vikao vya Bodi ya Usimamizi.*

**8.** Kumbukumbu za vikao vya Bodi ya Usimamizi zitathibitishwa na Bodi ya Usimamizi katika kikao kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

Kusita kuwa mjumbe.

**9.** Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi ya Usimamizi bila ya kuwa na sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu za afya ya kimwili au kiakili;

(d) ikiwa atasitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Bodi;

(e) ikiwa atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza mjumbe huyo; au

(f) kifo.

Kamati za Bodi ya Usimamizi.

**10.**-(1) Bodi ya Usimamizi inaweza, kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha Kamati kwa idadi itakayoona inafaa.

(2) Wajumbe wa Kamati zitakazoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, watakuwa miongoni mwa wajumbe wa Bodi ya Usimamizi au vyenginevyo kama itakavyoamuliwa na Bodi ya Usimamizi.

Kubainisha maslahi.

**11.**-(1) Mjumbe wa Bodi ya Usimamizi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kujadiliwa na Bodi ya Usimamizi, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi ya Usimamizi.

(2) Ubainishaji wa maslahi utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha maslahi:

(a) hatahudhuria katika majadiliano ya Bodi ya Usimamizi na kufanya uamuzi; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya uamuzi.

Kukasimu kazi za Bodi ya Usimamizi.

**12.**-(1) Bodi ya Usimamizi inaweza, pale itakapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati ya Bodi ya Usimamizi.

(2) Endapo Bodi ya Usimamizi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi hizo.

Posho.

**13.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi ya Usimamizi watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 15 Februari, 2024.

..........................................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***